JARIDA MAALUM LA

# USHIRIKA

**"Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo endelevu ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji"**




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati akifunga Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma*

## TOLEO MAALUM LA NANENANE 2024

# YALIYOMO

TUJENGE VYAMA VYA USHIRIKA VILIVYO IMARA - RAIS DKT. SAMIA..............03

WAKULIMA MSIWE NA MASHAKA NA MITAJI, NENDENI BENKI MKAPATE MITAJI - WAZIRI MKUU....02

RAIS DKT. SAMIA AUNGA MKONO MAGEUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI......02

WADAU WARIDHISHWA NA MAONESHO YA NANENANE KATIKA KIJIJI CHA USHIRIKA........05

CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA KDCU CHAJIVUNIA MAFANIKIO YAKE............05

TFC TAASISI MWAMVULI WA VYAMA VYA USHIRIKA......06

WADAU WA USHIRIKA WAELEZA FAIDA ZA MFUMO WA UNUNUZI KUPITIA MIZANI YA KIDIGITALI.....06

TAMCU LTD YAJIVUNIA KUTOA HUDUMA BORA KWA WANACHAMA NA WAKULIMA.......07

COASCO LAWAITA WANACHAMA WA SACCOS KUPATA ELIMU.....07

VYAMA VYA USHIRIKA NI SULUHISHO PEKEE LA KUJIKWAMUA KIUCHUMI - MRAJIS MSAIDIZI DODOMA...08-11

# TUJENGE VYAMA VYA USHIRIKA IMARA - RAIS DKT. SAMIA



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati akifunga Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameitaka Wizara ya Kilimo kuiangalia kwa jicho la kipekee Sekta ya Ushirika ili kujenga Vyama vya Ushirika vilivyo imara ili kurejesha hadhi na mchango wa Ushirika hapa nchini.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo Agosti 08, 2024 alipokuwa akifunga Maonesho ya Wakulima maarufu kama Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

"Ili mageuzi makubwa tunayoyafanya kwenye Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi yalete matokeo ya uchumi endelevu ni lazima tujenge Vyama vya Ushirika vilivyo imara; hivyo Wizara ya Kilimo naitaka itupie jicho kwenye Sekta hii ili kurejesha hadhi na mchango wa Ushirika nchini," amesema Mhe. Rais.



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe katika maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.***

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka Wakulima kutokuwa na hofu na mitaji kwakuwa Serikali inakwenda kuongeza upatikanaji wa Mikopo kwa riba nafuu kupitia taasisi mbalimbali za kifedha.
Kwa upande mwingine Rais Dkt. Samia amewahakikishia Wakulima upatikanaji wa Masoko na kutoa ruzuku ya mbegu kwa Wakulima na kuwataka kujisajili kwenye mfumo ili kunufaika kwa ruzuku hizo. "Lengo la Serikali ni kuwasaidia wakulima, ili waweze kujitegemea," amesema Mhe.Rais Dkt. Samia.




***Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, akikabidhi Hundi ya Malipo ya fidia kwa Wanaushirika wenye BIMA ya Mazao iliyotolewa na Benki ya NBC. Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, alipokea Hundi hiyo kwaniaba ya Wanaushirika wa Tumbaku walioathirika na Hali ya hewa katika mikoa ya Tabora, Katavi, Geita, Kigoma, Shinyanga na Mbeya.***

**WAKULIMA MSIWE NA MASHAKA NA MITAJI, NENDENI BENKI MKAPATE MITAJI - WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ametoa rai kwa wakulima wakiwemo Wanaushirika hapa nchini kutembelea Taasisi za kifedha kuweza kupata mitaji itakayoweza kuwasaidia katika shughuli mbalimbali za Kilimo, Uvuvi na Ufugaji na kupelekea kujikwamua kiuchumi.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa katika ufunguzi wa Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.




***Waziri Mkuu ameyasema hayo Agosti 01, 2024 alipokuwa akifungua Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane) katika Viwanja vya Nanenane Nzuguni Jijini Dodoma.***

"Wakulima msiwe na mashaka na mitaji, nendeni Benki mkapate mikopo ya masharti na riba nafuu, nendeni CRDB, NMB, NBC, MKOMBOZI na Taasisi zingine za kibenki, ukitaka kupata mtaji leo nenda benki, kila benki ina Afisa mmoja wa kuhudumia Wakulima na hii ni pamoja na wanaushirika nendeni benki mkapate mkopo" amesema Waziri Mkuu

Aidha, Waziri Mkuu amezitaka Sekta mbalimbali hapa nchini hususan Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ushirika kuimarisha Sekta hizo na kutumia teknolojia ya kisasa .

Waziri Mkuu amesema maonesho haya yanalenga kutoa fursa kwa Wakulima, Wafugaji, Wanaushirika, wajasiriamali na wasindikaji, kujifunza teknolojia mbalimbali kutoka kwa wadau wa Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Sekta binafsi na wataalamu walioko Serikalini, kuonyesha umuhimu wa Sekta hizo inavyoleta tija kwenye maisha ya kila mtu katika siku zote za maisha yake.

Maonesho haya ya Kimataifa ya Wakulima yameanza Agosti 01, 2024 na kilele chake kitakuwa Agosti 08, 2024.

**RAIS DKT. SAMIA AUNGA MKONO MAGEUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI**



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Maafisa Ugani na Wanaushirika katika kikao kilichofanyika Chamwino Ikulu Jijini Dodoma.***




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya Pamoja na Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kikao cha Maafisa Ugavi na Wanaushirika Chamwino Ikulu Jijini Dodoma.***

Akizungumza na Wanaushirika na Maafisa Ugani katika mkutano uliofanyika katika Ikulu ya Chamwino, Jijini Dodoma Agosti 10, 2024, Rais Samia amesema Vyama vya Ushirika ndiyo chombo madhubuti kinacholeta Maendeleo kwa watu wengi na kutondoa matabaka.



***Menejimenti ya TCDC, Warajis wasaidizi, wanaushirika na Maafisa Ugani wakiwa kwenye kikao na Mhe. Rais Dkt. Samia kilichofanyika Chamwino Ikulu Jijini Dodoma.***

"Serikali inawapongeza kwa uamuzi huu muhimu wa kuanzisha Benki yenu Wanaushirika; na Serikali itawaongezea Shilingi Bilioni tano (5) katika mtaji wa kuanzisha Benki hii muhimu kwa Wanaushirika na Wananchi kwa ujumla," amesema Mhe. Rais.

Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewapongeza Maafisa Ugani na watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kufanikisha nchi kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada.

"Wanaushirika mmeanza kufanya mabadiliko muhimu yanayohitajika, ninawapongeza na endeleeni kusimamia vema maslahi mapana ya Wanaushirika," amesema Mhe. Rais.




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika picha ya Pamoja na Maafisa Ugani Chwamino Ikulu Jijini Dodoma.***

Aidha, Mhe.Rais amewapongeza Wanaushirika kwa kuamua kuachangishana na kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika nchini, ambayo itakuwa ngao yao katika upatikanaji wa fedha za mitaji kwa Vyama na Wanaushirika.

**WADAU WARIDHISHWA NA MAONESHO YA NANENANE KATIKA KIJIJI CHA USHIRIKA**

Wadau mbalimbali wakiwemo Wakulima, Wafanyabiashara, wajasiriamali wameridhishwa na maonesho yaliyofanyika katika Banda la Ushirika maarufu kama "Kijiji cha Ushirika" katika maonesho ya Wakuluma (nanenane) yaliyofanyika kuanzia Agosti 01 hadi Agosti 08, 2024 Nzuguni Jijini Dodoma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wadau hao wamesema kuwa maandalizi yaliyofanyika katika banda hilo na kukuta watu wamejipanga muda wote kutuhudumia wananchi ni mazuri sana na yametusaidia kupata elimu mbalimbali kuhusu Ushirika, tunategemea kwa mwaka ujao yatakuwa mazuri zaidi kuliko haya.

Katika maonesho hayo Banda la Kijiji cha Ushirika lilikuwa limebeba wadau wa Ushirika wapatao kmkoa wa Dodoma, Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB),AGGRI – TERA, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko(COPRA), Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) Soko la Bidhaa Tanzania ( TMX), TAMFI, Chama Kikuu cha Ushirika cha Ziwa Nyasa (LATCU), ROTAI, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)Chama kikuu cha Ushirika wa Mazao Mkoa wa Ruvuma (MBIFACU), Chama Kikuu cha Ushirika cha Songea – Namtumbo (SONAMCU), Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Karagwe (KDCU) na Chama Kikuu cha Ushirika cha mkoa wa Kagera

Kupitia mabanda ya wadau wa Ushirika ndani ya Kijiji cha Ushirika, Wakulima, Wananchi,Wafugaji na Wajasiriamali waliweza kuapata elimu mbalimbali kuhusiana na Ushirika( KCU).

**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA KDCU CHAJIVUNIA MAFANIKIO YAKE**




***Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika – Karagwe (KDCU) Bw. Partson Josiah akizungumza wakati wa mahojiano maalum na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kwenye Maonesho ya Wakulima Nanenane Jijini Dodoma.***




***Mwenyekeiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) alipotembelea banda la Chama Kikuu cha Ushirika K.D.C.U kwenye maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.***

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Karagwe K.D.C.U kimesema kuwa kuwa hadi kufikia mwaka 2023 kimepata mafanikio makubwa sana ambayo yamepatikana kupitia wanaushirika wenyewe kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Chini ya Usimamizi Wizara ya Kilimo.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa Maadhimisho ya Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Mwenekiti wa Chama hicho Bw. Partson Josiah amesema kuwa moja ya mafanikio waliyoyapata ni kumiliki shule yao binafsi Nyaishozi Sekondari ambayo ndiyo shule ya kwanza kujengwa na wanaushirika hapa nchini.

Mafanikio mengine aliyoyataja ni pamoja na ujenzi wa ghala kubwa la kisasa linaloweza kuhifadhi magunia 6,000 ambapo kupitia ujenzi huo Mwenyekiti amemshukuru Dkt. Benson Ndiege Mrajis wa Vyama vya Ushitika na Mtendaji Mkuu wa TCDC kuwa bega kwa bega na kuwaruhusu kujenga ghala hilo.

"Namshukuru sana Dkt. Benson Ndiege kwa kutuunga mkono katika ujenzi wa ghala hili jippya na la kisasa linalochukua magunia yapatayo 6,000, tulipopeleka pendekezo la ujenzi wa ghala hakusita na alikuwa bega kwa bega hadi kukamilika kwa ujenzi huo.

Aidha,Mwenyekiti ameipongeza Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na mama Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuedelea kuona umuhimu wa Ushirika hapa nchini na kuiomba Wizara ya Kilimo kuendelea kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ili kuleta maendeleo makubwa kwa wakulima hapa hapa nchini.

Pia Chama kimeweza kupiga hatua kubwa zaidi kwa kuuza mazao kupitia Mfumo wa kMisasa wa ununuzi kupitia minada mabalimbali,mwenyekiti amesema kuwa kabla ya Mfumo kuanza kahawa iliuzwa sh,1,200 kwa kilo lakini baada ya matumizi ya mnada, kahawa inauzwa kwa kilo hadi kufikia sh, 5,200," hay ani mageuzi makubwa sana amesema Mwenyekiti.

Ameongeza kuwa, mbali na mafanikio hayo lakini pia KDCU imeajiri Maafisa Ugani kutoa huduma kwa AMCOS kwaajili ya kuwahudumia wakulima kuboresha zao la Kahawa. Pia KDCU inashirikiana na jamii kwa kusaidia utoaji wa misaada mbalimbali ikiwemo ujenzi wa vyoo mashulenki,kutoa huduma ya mashuka kwa wakinamama waliojifungua katika hospitali za Wilaya za Karagwe na Kyelwa na haya yote ni katika kutimiza msingoi namba saba (7) wa Ushirika wa kuijali jamii.

Vilevile amewashauri wakulima kutumia mizani ya kidigitali katika kuuza mazao yao

"Mizani ya kidigitali imekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wakulima,pale kabla ya Mfumo mpya wakilima walitumia mzani war ula ambao kwakweli wakulima walikuwa wakilalamika sana, ulikuwa unawaibia wakulima ulikuwa hauhesabu zile point, lakini baada ya mizani ya kidigitali unahesabu uhalisia kinachotoka shambani kwa mkulima kikaingia ghalani kinachoingia sokoni

jambo ambalo mkulima amenufaika na amekuwa akiamini Ushirika sana na kuona kuwa Ushirika ndio sehemu ambayo ni ya pekee ya kutatua changamoto za kimaisha na za kichumi"




***Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt. Abdulmajid Nsekela alipotembelea banda la KCBL Siku ya kilele cha maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.***

**TFC TAASISI MWAMVULI WA VYAMA VYA USHIRIKA**

Shirikisho la Vyama vya Ushirika ni Taasisi Mwamvuli ya Vyama vya Ushirika, ikiwa na kazi ya kutetea Vyama vya Ushirika,kufanya ushawishi na utetezi kwa Vyama vya Ushirika na kutafuta maendeleo ya Vyama vya Ushirika.



***Afisa Uhamasishaji na Masoko – TFC Emmanuel Ndanda akizungumza wakati wa mahojiano maalum na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa Maonesho ya Wakulima.***

Hayo yamebainishwa na Emmanuel Danda Afisa Uhamasishaji na Masoko TFC wakati wa mahojiano maalumu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa Monesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa Jijini Dodoma.

Aidha Bw. Ndanda ameongeza kuwa kuna ngazi tatu za Vyama vya Ushirika ambapo ngazi ya kwanza ni Vyama vya Msingi yaani AMCOS,Ngazi ya pili ni Chama Kikuu cha Ushirika na ngazi na ngazi ya tatu na a mwisho ni chama Kilele cha Ushirika Katika ngazi zote tatu kuna Vyama vinavyojishughulisha na Vinajishughulisha na kilimo cha mazao,Wavuvi na Mifugo

Shughuli zingine zinazofanywa na TFC ni kuwajengea uwezo kupitia mafunzo mbalimbali,kufanya marketing linkage (uhusiano wa kimasoko), uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika kupitia majukwaa mbalimbali ya vyama vya Ushirika ya kitaifa na kimataifa kama vile Siku ya Ushirika Duniani (SUD).

Ameongeza kuwa, TFC ndio muasisi wa uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ambako mchakato wake unakaribia kukamilika hivi karibuni lakini pia inaendelea na kuhamasisha shughuli mbalimbali zinazoleta kuleta tija ya uzalishaji na biashasha.

Kupitia maadhimisho ya Wakulima; TFC imetoa elimu mbalimbali kuhusiana na dhama ya ushirika, historia ya ushirika,dira ya ushirika,mbali na mafunzo.

**WADAU WA USHIRIKA WAELEZA FAIDA ZA MFUMO WA UNUNUZI KUPITIA MIZANI YA KIDIGITALI**

Wadau mbalimbali wa Ushirika wamekuwa na mtazamo Chanya kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kiditali wa ununuzi wa mazao kupitia minada mbalimbali ya mazao inayofanyika katika Vyama vyao vya Usshirika kupitia Mfumo wa Stakabadhi za ghala.

Wakieleza kwa nyakati tofauti katika mahojiano maalum na kitengo cha mawasiliano Serikalini wameeleza kwa Mfumo wa Stakabadhi za ghala na mizani ya kidigitali wa ununuzi wa mizani kupitia kinada mbalimbali imekuwa mkombozi na msaada mkubwa sana kwa wakulima kwani wakulima wanauza mazao kwa bei ya juu wanayoitaka wao na mizani ya kisasa inapima mazao kwa uhalisia ukilinganisha na mfumo wa zamani ambao ulikuwa ukiwapunja wakulima.



***Wananchi na Wanaushirka wakifuatilia Mafunzo yaliyotolewa na TMX katika Maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.***

"Mizani ya kidigitali imekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wakulima,pale kabla ya Mfumo mpya wakilima walitumia mzani war ula ambao kwakweli wakulima walikuwa wakilalamika sana, ulikuwa unawaibia wakulima ulikuwa hauhesabu zile point, lakini baada ya mizani ya kidigitali unahesabu uhalisia kinachotoka shambani kwa mkulima kikaingia ghalani kinachoingia sokoni jambo ambalo mkulima amenufaika na amekuwa akiamini Ushirika sana na kuona kuwa Ushirika ndio sehemu ambayo ni ya pekee ya kutatua changamoto za kimaisha na za kichumi" ameeleza mwenyekiti wa KDCU Bw.Partson Josiah

" kwakweli hili tumelipokea vizuri na haijawahi kutokea,kwa mfano kama kwetu Kagera kahawa ya Maganda imeweza kufikia shilingi elfu tano (5,000) kitu ambacho haijawahi kutokea,kwahiyo tunawaelimisha wananchi waendelee kuleta Kahawaza minadani,vilevile wazingatie ubora kwasababu kahawa isipokuwa bora yule aliyenunua kwa shilingi elfu tano hatonunua, wavune kahawa iliyokomaa,waanike vizuri ili kuweza ili kuweza kendana na unyevu" ameeleza Bw. Partson

Naye Kaimu Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbinga (MBIFACU) Faraja Michael amesema kuwa kupitia minada umeweka uwazi mkubwa kati ya mnunuzi Wakulima na Viongozi tofauti na minada ile ya kizamani iliyokuwa inafanyika kwa mabox na minada ya kidigitali ambayo inatoa uwanja mpana zaidi kwa wakulima kuona uwazi kabisa kuwa bei tunazozipata kwenye minada ni bei stahiki kabisa

## TAMCU LTD YAJIVUNIA KUTOA HUDUMA BORA KWA WANACHAMA NA WAKULIMA




***Afisa Kilimo wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kilimo na Masoko (TAMCU) Mustapha Abdallah Mawenje akifanya mahojiano na Kitengo cha Mwawasiliano Serikalini wakati wa Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.***

Chama Kikuu cha Ushirika wa Mazao na Masoko TAMCU LTD kimepata mafanikio makubwa kupitia Ushirika ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bora kwa wanaushirika,wakulima, wananchi na jamii inayowazunguka.

Afisa Kilimo wa TAMCU Mustapha Abdallah Mawenje ameeleza kuwa wanajivunia kuwahudumia wakulima na wanachama kwa kutoa elimu bora na endelevu kwa wanachama,kutoa elimu bora ya mafunzo,kutoa pembejeo za Kilimo na mafunzo kwa gharma nafuu,kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao kwa wakulima na wanachama,kutafuta masoko ya uhakika na kuiinua jamii kiuchumi na kijamii na kuimarisha Maisha yao

Ameongeza kuwa Pamoja na huduma bora wanazitoa kwa wanachama na wakulima lakini pia malengo ya TAMCU ni kuwashawishi wakulima kujiunga na Ushirika,kuwa kitovu cha utafutaji wa masoko ya uhakika,utekelezaji wa miradi mbalimbali kama vile uanzishwaji wa mashamba,kuendeleza ardhi,majengo na ununuzi wa magari.

Akitaja mafanikio waliyoyapata ni Pamoja na kuwafika ia wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuwahudumia kwenye Wilaya ya Tunduru na kuwahakikishia Masoko ya uhakika wa bidhaa zao,kufanikisha mradi wa ghala kuu lenye thamani ya mil. 490 ambalo hutumika kuhifadhia mazao ya wanachama na kusubiri kwaajili yam nada na kutoa elimu ya ugani kwa wakulima na wanachama

Aidha ametoa wito kwa wakulima kwa wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kuweza kunufaika na mambo mbalimbali ikiwa ni Pamoja na kuwa na nguvu ya Pamoja kupata mikopo,kupata pembejeo za Kilimo kwa urahisi,urahisi wa kuunganishwa na taasisi mbalimbali na kuweza kupata mikopo ya magari na matrekta yanayoweza kuwasaidia katika kuwasaidia kujiongezea nguvu ya kiuchumi na kukuza kipato chao.

## COASCO LAWAITA WANACHAMA SACCOS KUPATA ELIMU

Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Golden Kajaba ameabainisha majukumu mbalimbali yanayofanywa na Shirika la la Ukaguzi na Usimamizi (COASCO) na kutoa wito kwa Wanachama wa SACCOS kujifunza namna ya kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata miongozo ya kimataifa pamoja na utawala bora ili kuhakikisha Vyama vyao vinafanya vizuri na kupata hati safi.

Kajaba ameyasema hayo wakati akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa Mahojano Maalum wakati wa Maonesho ya Wakulima nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma. "Kazi kubwa za COASCO ni ukaguzi wa Vyama vya Ushirika,kusimamia makampuni ambayo yanauwezo wa kukagua Vyama vya Ushirika,Kufanya tafiti na kutoa ushauri kwa Vyama vya Ushirika mbalimbali na kuandalia miongozo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuviwezesha Vyama kufanya vizuri"

Kajaba ameongeza kuwa ili Kuhakikisha kuwa wanatoa mafunzo kwa Vyama vya Ushirika namma ya kutumia miongozo inayotumika katika uandaaji wa taarifa za fedha kuhakikisha kuwa Vyama hivyo vinafanya vizuri na kupata hati safi ni vizuri wakapata mafunzo kupitia COASCO ili kuepukana na hati zisizoridhidhisha.

"tangu tumeanza kutoa elimu kumekuwa na ongezeko kubwa la Vyama kupata hati zinazoridhisha ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita"

## VYAMA VYA USHIRIKA NI SULUHISHO PEKEE LA KUJIKWAMUA KIUCHUMI – MRAJIS DODOMA

Mrajis wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Dodoma amesema kuwa Vyama vya Ushirika vimekuwa kama Daraja la Wananchi kujikwamua kichumi na kutoa wito wa Wananchi hasa Wakulima,Wafugaji na Wavuvi kujiunga na vyama hivyo




**Mrajis wa Vyama vya Ushirika wa mkoa wa Dodoma Joseph Chitinka akiwa katika mazungumzo maalum na kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa maadhimisho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.**

Ameyasema hayo Agosti 04,2024 wakati wa mahojiano maalumu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa Maonesho ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika Jijini Dodoma. "Wakulima baada ya kulima wanaweza kuja kuweka fedha zao kwenya Vyama vya Akiba na Mikopo lakini pia wanaweza kujiendeleza likawa kama ndio suluhisho kwao la kujipatia mitaji na kujiendeleza kimaisha " amesema Chintinka.

Katika mahojiano hayo,Mrajis alieleza kuwa katika mkoa wa Dodoma kuna jumla ya Vyama vya Ushirika 128,Vyama vya Msingi (AMCOS) vikiwa ni 38 na Vyama 90 ni vya Akiba ya mikopo yaani SACCOS.

Amesema Vyama hivyo vimekuwa mtetezi wa wanyonge,vimekuwa sehemu ya kukuza mtaji na kimbilio la kupata soko la Pamoja,wakulima na wajasiriamali wamekuwa wakizalisha na kuuza kwa pamoja kwa kufuata miongozo mbalimbali inayotolewa kwenye masoko na hivyo kuuza mazao na bidhaa zao kwa bei inayoridhisha.

Aidha ametoa wito kwa Wakulima,Wafugaji na Wafugaji,Wajasiriamali na makundi mengine yanayojishughulisha na shughulu mbalimbali kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kuweza kuwa na nguvu ya Pamoja na kuweza kujikwamua kiuchumi.



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania - TCDC Dkt. Abdulmajid Nsekela katika picha ya Pamoja na Makamishna wa TCDC na watumishi wa TCDC katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe wakati akitembelea mabanda mbalimbali wakati wa maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akisalimiana na Viongozi wa Chama na Serikali wakati alipowasili katika viwanja vya Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akisalimiana na Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule wakati alipowasili katika viwanja vya Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mrajis Msaidizi (Uhamasishaji) akisalimiana na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika wakati alipotembelea mabanda mbalimbali kayika Kijiji cha Ushirika kwenye Maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.*




*Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TCDC Gabriel Mwita akisalimiana na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC Dkt.Benson Ndiege katika Maonesho ya Wakulima Jjijini Dodoma.*



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege, Mkurugenzi – WRRB Asangye Bangu, Meneja wa Benki ya KCBL Godfrey Ng'urah wakiwabadilishana Mawazo wakati wa Maonesho ya Wakulima ( Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania TCDC Dkt. Abdulmajid Nsekela alipotembelea banda la Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI katika maadhimisho ya Wakulima Jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa COPRA na Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya TCDC katika mazungumzo na Mkuu wa mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Meneja wa Benki ya KCBL na Kamishna wa TCDC Godfrey Ng'urah katika picha ya Pamoja na Viongozi wa Vyama vya Ushirika katika maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*



*Wananchi walipotembelea laBanda la bidhaa za Mwani katika Kijiji cha Ushirika kwenye Maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*



*Naibu Mrajis (Uhamasishaji) Consolata Kiluma akimsikiliza Mratibu, Ofisi ya Dodoma ya Chuo kikuu Cha Ushirika Moshi Bahati Rukiko kutoka kwa katika banda la Chuo cha Ushirika (MoCU) katika maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*



*Afisa Masoko wa TFC Emmanuel Danda akitoa elimu kuhusu Ushirka katika Maonesho ya Wakulima ( Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma alipotembelea mabanda mbalimbali katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma Joseph Chintinka na Mrajis Msaidizi (Uratibu na Uhamasishaji) Ibrahim Kadudu wakibadilishana mawazo katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mkaguzi – COASCO Elice Mmari akizungumza na mmoja wa wadau alipotembelea banda la COASCO katika Kijiji cha Ushirika wakati wa Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt. Abdulmajid Nsekela wakisalimiana na Kamishna wa TCDC Richard Mayongela katika maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*




*Wadau wa Ushirika wakitangaza na kuuza bidhaa zao katika banda la KCBL katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma*



*Afisa Ushirika Mkuu Deogratius Bendera akisalimiana na mdau wa Ushirika katika Banda la Ushirika katika Kijiji cha Ushirika kwenye Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini DOdoma.*




*Mdau wa Ushirika Betty Mwasongwe akipata elimu ya Ushirika kwenye banda la Bodi ya Pareto Tanzania wakati wa Maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamishna ya TCDC Dkt. Abdulmajid Nsekela akipata maelezo katika banda la LATCU kwenye maonesho ya Wakulima (Nanenane) Jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzani Dkt. Abdulmajid Nsekela alipotembelea banda la TTCL Siku ya Kilele cha Maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma*




*Mwenyeketi wa Chama Kikuu - KDCU Partson Josiah alipotembelea banda Korosho Joint Enterprises Ltd kujionea bidhaa mbalimbali zinazopatikana katika banda hilo katika maonesho ya Wakulima Jijini Dodoma.*

# USHIRIKA

Pamoja Tujenge Uchumi

## MAKAO MAKUU YA TUME


Mtaa wa Kuu, S.L.P 201 Dodoma
+255 026 - 2322456
+255 026 - 2321973
ushirika@ushirika.go.tz
www.ushirika.go.tz
ushirika_tcdc
Tume ya Maedeleo ya ushirika